15273823

# THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# KJSEA 2025

## KISWAHILI

15273823

902/1 **(Lugha)** Karatasi 1

**Okt. 2025 - Muda: Saa 1 Dakika 40**

### MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Umepewa **kijitabu** hiki cha maswali na **karatasi ya majibu**. Kijitabu hiki kina maswali **50.**
2. Jibu maswali **yote** kwenye **karatasi ya majibu** uliyopewa kujibia maswali na wala **sio** katika kijitabu hiki.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
4. Tumia penseli ya kawaida (HB).
5. Hakikisha kuwa **karatasi ya majibu** uliyopewa imejumuisha yafuatayo:
   **NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
   **JINA LA SOMO**
6. Kwa kila swali, **1 - 50**, umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A**, **B**, **C** na **D**. Herufi hizi zimeandikwa ndani ya viduara. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
7. Kwenye karatasi ya majibu, lionyeshe jibu sahihi kwa kujaza kiduara chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu, ukitumia penseli.
8. Usitie alama zozote nje ya viduara. **Thibitisha jibu lako kabla ya kujaza kiduara ulichochagua.**

   **Mfano:**

   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **25.** Orodha ifuatayo ni ya majina ya vitu vinavyopatikana katika mazingira yako. Ni jibu lipi lenye vitu vinavyotajwa na nomino za ngeli ya I-ZI?

   A. kucha, sahani
   B. kuta, ngoma
   C. nyuta, kamba
   D. pamba, taa

   Jibu sahihi ni D.

   **Katika karatasi ya majibu:**

   Katika viduara vinavyoonyesha majibu ya swali namba **25**, jaza kiduara chenye herufi **D** kwa kutumia penseli.

   **25.** (A) (B) (C) ●

9. Jaza kiduara chako vizuri, **KIWE CHEUSI** na alama zisijitokeze nje ya kiduara.
10. Kwa kila swali, jaza **kiduara kimoja tu** kati ya viduara vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 10 zilizopigwa chapa.**
**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa na maswali yote yapo ipasavyo.**

© 2025, The Kenya National Examinations Council



Geuza ukurasa

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 6.*

Sonita alitembea halahala kuelekea nyumbani kutoka shuleni. Alikuwa ameagana na wanafunzi wenzake na kila mtu akashika njia ya kwao. Mwendo wa kutoka mahali alipokuwa hadi kwao haukuwa mrefu. Sonita alitamani kufika nyumbani apumzike kwani alikuwa amechoka. Siku hiyo, alikuwa ameshiriki michezo shuleni. Ghafla bin vuu mawazo ya Sonita yalitekwa na sauti ya mtoto mchanga.

"Ala! Sauti ya mtoto? **Mtoto anafanya nini peke yake kando ya barabara?**" Maswali haya na mengine mengi yalimjia Sonita kwa wakati mmoja.

Sonita alinyatia na kuchungulia ilikotoka sauti hiyo. Alipigwa na bumbuazi kumwona mtoto mchanga amefungwafungwa kwa nguo za mararu na kutiwa ndani ya kapu kuukuu. Moyo ulimpapa. Hakujua afanye nini. Sonita aliamua kutimua mbio ili kukikwepa kioja hicho lakini kabla ya kufanya hivyo, aliyaona mengine mbele yake. Jibwa kubwa lilikuwa limelala nyuma ya kapu hilo. **Lilikuwa limetulia kama maji mtungini.** Sonita alidhani kuwa bila shaka azma ya jibwa hilo ilikuwa moja, kumtafuna mtoto yule. Alinyakua kapu hilo na kukimbia. Jibwa lilimwangalia kwa jicho la pembeni. Lilibaki pale likinusanusa. Sonita alifika nyumbani akihema kwa mshtuko.

"Sijui nimfanyie nini mtoto huyu? Baba na mama hawajafika nyumbani. Mtoto mwenyewe anahitaji chakula, mavazi na malazi. Afadhali niwapigie wazazi wangu simu waje haraka. Jukumu hili siliwezi peke yangu." Sonita alisema huku akimfunika mtoto kwa blanketi ili aache kutetemeka. Mtoto mwenyewe hakulia bali alirambaramba midomo, ishara ya kutafuta riziki ya tumboni.

Wazazi wa Sonita waliwasili nyumbani haraka. Walipishana kwa sekunde tu. Aliwaeleza yote yaliyojiri. Mama alimshughulikia mtoto vyema. Alimwosha, akamfunga vizuri kwa nguo safi na kumnywesha maziwa. Mtoto alilala usingizi wa pono. Baba na Sonita nao walishika njia hadi kwenye kituo cha polisi kuripoti tukio hilo.

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

**1.** Kulingana na aya ya **kwanza**, Sonita alitembea haraka kuelekea nyumbani ili
   - A. kufika nyumbani mapema kama wenzake.
   - B. kuonyesha kuwa kwao kulikuwa karibu.
   - C. kupata nafasi ya kuondoa uchovu.
   - D. kutambua ilikotoka sauti aliyoisikia.

**2.** Mawazo ya Sonita katika aya ya pili '**Mtoto anafanya nini peke yake kando ya barabara?**' yanadhihirisha nini kuhusu jamii ya Sonita?
   - A. Wanafunzi wengi ni wadadisi wa mambo katika mazingira yao.
   - B. Sio kawaida kumpata mtoto ameachwa barabarani.
   - C. Watu wengi wamezoea kuwaacha watoto barabarani.
   - D. Baadhi ya watu hujishughulisha na mambo yanayowahusu pekee.

**3.** Chagua jibu linaloonyesha kuwa Sonita ni mwenye maadili.
   - A. Alitembea haraka ili afike nyumbani.
   - B. Alijiuliza maswali mengi ili kujua ukweli.
   - C. Alifikiria kumuokoa mtoto asiliwe na jibwa.
   - D. Alimfunika mtoto ili aache kutetemeka.

4. Chagua jibu linaloonyesha mfuatano sahihi wa matukio katika kifungu.
   (i) Sonita kuwapigia wazazi simu.
   (ii) Sonita kuwaeleza yaliyojiri.
   (iii) Sonita kuagana na wenzake.
   (iv) Sonita kunyakua mtoto.

   A. (iii) (iv) (i) (ii)
   B. (iv) (iii) (ii) (i)
   C. (iii) (i) (ii) (iv)
   D. (iv) (ii) (i) (iii)

5. Kauli, '**lilikuwa limetulia kama maji mtungini,**' imetumia tamathali gani ya usemi?
   A. Nahau
   B. Sitiari
   C. Tashbihi
   D. Methali

6. Je, unafikiri polisi walichukua hatua gani baada ya kisa cha mtoto kuripotiwa?
   A. Walianza kuwatafuta wazazi wa mtoto.
   B. Walimchukua mtoto na kumweka kituoni.
   C. Waliwaleta watoto wengine waliokuwa wamepotea.
   D. Waliwapatia zawadi waliofika kupiga ripoti.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la* **7** *hadi la* **12**.

Zakaria alikutana na Kiberenge njiani. "Unaenda wapi?" Kiberenge alimuuliza Zakaria. "Hakuna hata salamu bwana?" Zakaria alimuuliza Kiberenge.

"Sina muda wa salamu. Nachelewa. Nataka kwenda kupanga meza zangu. Wateja wangu wanakaribia kutoka kazini. Kwanza, naomba univunjie noti hii." Kiberenge alisema akiwa na haraka huku akimpatia Zakaria noti ya mia tano. Zakaria aliwaza na kuwazua. Hakujua amvunjie Kiberenge pesa au la. Hakumwamini Kiberenge hata kiduchu. Alimfahamu Kiberenge ndani nje. Kiberenge hakuwa mtu mwenye maadili. Alitumia kila fursa aliyopata kuwalaghai watu.

"Haidhuru!" Zakaria alijisemea na kumpa Kiberenge pesa alizohitaji. Kiberenge alizipokea pesa hizo huku akicheka na kutoa gego la mwisho.

Haukupita muda mrefu, Zakaria akafika dukani akiwa na haja ya kununua bidhaa. Alishangaa alipoambiwa kuwa pesa alizokuwa nazo zilikuwa bandia. Alirudisha mawazo nyuma na kusema, "Ala! Kumbe Kiberenge amenichezea. Sawa tu. Leo atampata pwaguzi." Zakaria alifululiza moja kwa moja hadi mahali ambapo Kiberenge alichezeshea watu kamari. Alitumaini kuwa angempata kwani mara nyingi alikuwa akijificha asikamatwe na askari kanzu.

Zakaria alimkuta Kiberenge akiwashawishi wapita njia kucheza kamari. Aliwaita kwa sauti, "Njooni magwiji. Haraka yako ndio bahati yako. Hapa pesa zako zitazaa pacha."

Zakaria alijibanza pembeni na kutafuta kwenye mtandao nambari ya kituo cha polisi kilichokuwa karibu. Aliipata na **kuwataarifu** kuhusu uhuni wa Kiberenge. Polisi walimshauri Zakaria kujidai kuwa alitaka kucheza kamari. Walimwambia atumie pesa ghushi alizopewa na Kiberenge. Zakaria alifululiza kwenda kucheza kamari kama alivyoshauriwa.

Kiberenge alimkaribisha Zakaria kwa mikono miwili. Zakaria naye hakusita; alianza kucheza mara moja kwa pesa bandia. "Hahaha! umeliwa. Wajinga ndio waliwao. Wekelea pesa zaidi ili ukomboe zilizopotea." Kiberenge alisema huku akicheka kama fisi.

Kicheko cha Kiberenge kiligeuka kilio askari kanzu walipowasili wakiandamana na askari polisi. Askari hawa waliwazingira Kiberenge na wachezaji kamari wenzake. Zakaria alisimama kando tu na kujionea sinema.



Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

7. Kulingana na kifungu, Kiberenge hakumwamkua Zakaria kwa sababu alikuwa na
   A. wateja wengi waliokuwa wanamsubiri.
   B. haraka ya kufungua biashara yake.
   C noti aliyotaka kuvunjiwa.
   D. swali ambalo alitaka kujibiwa.

8. Ni jibu lipi linaonyesha uhusiano kati ya Zakaria na Kiberenge?
   A. Walikuwa na mazoea ya kuvunjiana pesa.
   B. Kiberenge alipenda kusaidiwa na Zakaria.
   C. Walikuwa na urafiki wa dhati.
   D. Zakaria alijua mienendo ya Kiberenge.

9. Neno **'kuwataarifu'** limetumiwa katika kifungu. Chagua kisawe cha neno hilo.
   A. kuwakumbusha
   B. kuwajulisha
   C. kuwasisitizia
   D. kuwapendekezea

10. Je, unadhani Kiberenge alifanya nini baada ya kukamatwa na askari?
    A. Aliwaita wateja aliokuwa anacheza nao kamari.
    B. Alitaka kumrudishia Zakaria pesa bandia.
    C. Alikubali na kuandamana nao hadi kituoni.
    D. Aliwafundisha askari jinsi ya kucheza kamari.

11. Chagua methali ambayo inaweza kutumiwa kumshauri Kiberenge.
    A. Siku za mwizi ni arubaini.
    B. Usiache mbachao kwa msala upitao.
    C. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
    D. Kidole kimoja hakivunji chawa.

12. Chagua jibu ambalo **si** kichwa mwafaka kwa kifungu hiki.
    A. Kuwajibika kwa wanajamii.
    B. Biashara za mjini.
    C. Manufaa ya maamkuzi.
    D. Udanganyifu haufai.

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 13 hadi la 17.*

Haki ndio msingi wa mahitaji yote ya kila mtu. Mahitaji hayo ni kama vile: lishe bora, mavazi, malazi na elimu. Swali ni je, ni nani anayefaa kuwatimizia watu haki zao?

Watu tofauti hupata haki zao kupitia njia mbalimbali. Watoto kwa mfano hutimiziwa haki zao na wazazi, walezi au walimu wao. Kwa upande mwingine, wakongwe hutimiziwa mahitaji yao na wana wao na jamii kwa jumla.

Kunayo mambo mengi ambayo huathiri upataji wa haki za kibinadamu. Mambo hayo ni kama vile sheria na sera za jamii fulani. Jamii inayowajali watu wake huweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa kila mwanajamii anapokea haki zake. Taratibu hizi huwalinda wanajamii dhidi ya **dhuluma** zinazotokana na ukiukaji wa haki za kibinadamu kama vile ukosefu wa elimu.

Haki za kibinadamu zinapokiukwa jamii hutamauka na kufarakana. Watu huanza kuvunja sheria na kuwadhulumu wenzao. Wengine huwatumia vibaya watu wasio na uwezo wa kiuchumi ndiposa wawatimizie angalau baadhi ya mahitaji yao.

Kumnyima mtu haki yake ni kumnyima ubinadamu wake. Ni kumfanya mtu kuwa zuzu asiyewaza chochote bali kutii analoambiwa bila kuhoji. Jamii kamili ni ile ambayo inatimiza haki za kila mwanajamii na kuzilinda kwa jino na ukucha.

**13.** Kulingana na kifungu,
- A. wazee huwa na mahitaji mengi zaidi katika jamii.
- B. watu wote wana jukumu la kuwatimizia watoto haki zao.
- C. kuna njia maalum za kushughulikia mahitaji ya wanajamii.
- D. kila mwanadamu anastahili kupata vyakula vyenye virutubishi.

**14.** Kuwatimizia wakongwe haki zao ni njia moja ya kukuza
- A. kusameheana.
- B. bidii.
- C. makini.
- D. uwajibikaji.

**15.** Chagua jibu ambalo ni sahihi kwa mujibu wa kifungu.
- A. Jamii ikikosa kutekeleza haki, watu hupotoka kimaadili.
- B. Wanajamii huzungumza mambo mengi kuhusu haki zao.
- C. Haki za watu hufikiriwa na wanajamii wenyewe.
- D. Ukosefu wa haki hutegemea tofauti za kiuchumi.

**16.** Ukiukaji wa haki za kibinadamu husababisha
- A. wanaonyimwa haki kuwa mazuzu.
- B. uundaji wa sheria na sera mpya.
- C. kuzoroteka kwa hali ya uchumi.
- D. wanajamii kuzilinda mali zao.

**17.** Kulingana na kifungu, maana ya neno **dhuluma** ni
- A. makosa.
- B. uonevu.
- C. chuki.
- D. hasara.

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la **18** hadi la **20**.*

Wanafunzi wa shule ya Junia huwa na ratiba ya Klabu mbalimbali kila siku ya wiki kama ilivyo kwenye jedwali lifuatalo:

| **Klabu** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** |
|---|---|---|---|---|---|
| Skauti | ✓ | ✓ | | ✓ | |
| Michezo | | | ✓ | | |
| Densi | ✓ | | | ✓ | |
| Majadiliano | ✓ | ✓ | | ✓ | ✓ |
| Kilimo | | | ✓ | | ✓ |
| Mazingira | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Upishi | | ✓ | | | ✓ |

**18.** Chagua jibu linaloonyesha wanaklabu wanaokutana mara mbili pekee kwa wiki.

A. Upishi, skauti, densi

B. Densi, skauti, majadiliano

C. Upishi, kilimo, densi

D. Kilimo, densi, majadiliano

**19.** Ni siku gani wanafunzi wa shule ya Junia hushiriki katika klabu chache zaidi?

A. Jumanne

B. Jumatano

C. Alhamisi

D. Ijumaa

**20.** Chagua jibu linaloonyesha klabu ambayo wanafunzi hushiriki kila siku ya wiki.

A. Kilimo

B. Majadiliano

C. Mazingira

D. Upishi

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la **21** hadi la **25**.*

*(Ni uwanjani. Wanafunzi wanafanya mazoezi ya mwili. Tezi na Nira wanakimbia polepole huku wakizungumza.)*

Tezi: *(Akimsogelea.)* Hali vipi Nira?

Nira: Nzuri sana dada. Nawe waendelea vipi?

Tezi: *(Kwa furaha.)* ___**21**___. Ninaendelea kufanya mazoezi. Si unajua ni wakati wa matayarisho ya michuano ya futiboli? Timu yetu inajikaza kisabuni. Unajua, ajizi ni ...

Nira: *(Akidakia.)* Nyumba ya njaa, eti. Hata sisi tunajikakamua.

Tezi: *(Akihema.)* Hapo sawa mwenzangu! Mwaka jana tulinyakua kombe. Tunatumai mwaka huu pia tutalileta kwetu. Wavulana wote wameamua liwe liwalo, ushindi utabaki kwetu.

Nira: Hali kadhalika, kwa upande wa timu yetu, mabanati hawalali. Tumeamua kuwa sharti tulinyakue kombe mwaka huu. Mwaka jana lilitupita.

Tezi: *(Akipunguza mwendo.)* Wacha nipumue kidogo. Nimekimbia kwa muda mrefu; moyo wangu unadunda. Nikiendelea hivi nitaanguka.

Nira: *(Akisimama.)* ___**24**___. Hakika hata mimi ninahitaji kupumzika sasa. Kwaheri. Tutaonana kesho tena.

Tezi: *(Akimtazama.)* Nami nitakufuata punde.
*(Wanaagana.)*

**21.** Chagua jibu lenye kauli sahihi kujaza nafasi ya **21** katika kifungu.
- A. Napenda hivyo.
- B. Ni mzima.
- C. Ndio hali.
- D. Nafurahi kukuona.

**22.** Chagua maneno yanayoonyesha kuwa Nira aliweza kukamilisha kauli ya Tezi wakati wa mazungumzo.
- A. Tutaonana kesho tena
- B. Nyumba ya njaa
- C. Mwaka jana tulinyakua kombe
- D. Wacha nipumue kidogo

**23.** Ni yepi kati ya maneno yafuatayo yanayoonyesha kuwa wahusika walikuwa na uhusiano wa karibu?
- A. Hapo sawa mwenzangu
- B. Mwaka jana lilitupita
- C. Timu yetu inajikaza
- D. Nami nitakufuata punde

**24.** Chagua neno ambalo Nira angetumia katika nafasi ya **24** kwenye mazungumzo.
- A. Basi
- B. Pole
- C. Kunradhi
- D. Tafadhali

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

25. Ni ishara gani ambayo Nira alistahili kutumia alipomuaga Tezi?
A Kutikisa kichwa
B. Kuinua mabega
C. Kupepesa macho
D. Kumpungia mkono

*Kifungu kifuatacho kina nafasi 26 hadi 35. Chagua jibu **lifaalo zaidi** kujaza nafasi kati ya majibu manne uliyopewa baada ya kifungu.*

"Daktari __26__ tembe za kumezea hapa na __27__ za kubeba." Muuguzi alimweleza Topasa. "Hakikisha kuwa __28__ mara tatu kwa siku," aliendelea muuguzi.

__29__ Ninafahamu kuwa __30__ maradhi ni ghali kuliko kuyazuia." Topasa alijibu kwa sauti ya unyonge.

Topasa __31__ unyounyo huku amebeba bahasha ya dawa na kuelekea nyumbani. Kwa siku tano __32__, Topasa __33__ maagizo ya dakari. Alikula chakula chenye virutubishi __34__ kumeza dawa. __35__ kazi ngumu, alipumzika nyumbani.

| | A. | | B. | | C. | | D. | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 26. | A. | amekupatia | B. | akikupatia | C. | angekupatia | D. | akakupatia |
| 27. | A. | kingine | B. | mingine | C. | nyingine | D. | lingine |
| 28. | A. | anameza | B. | unameza | C. | tunameza | D. | mnameza |

29. A. "Nitazingatia maagizo yako, muuguzi.
B. "Nitazingatia maagizo yako, muuguzi?
C. "Nitazingatia maagizo yako, muuguzi!"
D. "Nitazingatia maagizo yako, muuguzi."

| | A. | | B. | | C. | | D. | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 30. | A. | kuambua | B. | kuchunguza | C. | kufahamu | D. | kutibu |
| 31. | A. | alitembeleana | B. | alitembelea | C. | alitembea | D. | alitembelewa |
| 32. | A. | zilivyofuata | B. | zilizofuata | C. | zilikofuata | D. | zilipofuata |
| 33. | A. | alitia bidii | B. | alitia hamu | C. | alitia fora | D. | alitia maanani |
| 34. | A. | kabla ya | B. | fauka ya | C. | badala ya | D. | ndani ya |
| 35. | A. | Hutafanya | B. | Hukufanya | C. | Hatafanya | D. | Hakufanya |

*Kutoka swali la 36 hadi la 50, chagua jibu sahihi.*

36. Maneno **bao** na **mbao** yana sauti zinazokaribiana. Je, ni neno lipi lenye sauti zinazokaribiana kimatamshi na neno **dhamani**.
A. samani
B. thamani
C. jamani
D. ramani

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

37. Chagua jibu lenye maana kuwa **'Katu alisafisha chumba kwa niaba ya Bili.'**
A. Katu na Bili walisafisha chumba.
B. Katu alisafishiwa chumba cha Bili.
C. Katu alimsafishia Bili chumba.
D. Katu na Bili walisafishiwa chumba.

38. Chagua kiambishi sahihi kukamilisha nafasi katika sentensi ifuatayo:
Ngozi nyeusi ___litumiwa kutengeneza viatu hivi.
A. zi
B. ya
C. vi
D. wa

39. Karisa alipofika alipata Lulu ameondoka mapema. Kwa hivyo,
A. Karisa alifika kwani alipata Lulu ameondoka mapema.
B. Karisa alifika lakini alipata Lulu ameondoka mapema.
C. Karisa alifika pia alimpata Lulu ameondoka mapema.
D. Karisa alifika lau alimpata Lulu ameondoka mapema.

40. Chagua sentensi ambayo ni **ukanusho** wa sentensi ifuatayo:
**Juma angemaliza mtihani wake angepata cheti.**
A. Juma asipomaliza mtihani wake hatapata cheti.
B. Juma hajamaliza mtihani wake hatapata cheti.
C. Juma asingalimaliza mtihani wake asingalipata cheti.
D. Juma asingemaliza mtihani wake asingepata cheti.

41. Leona alimfanya Toni aandike barua ya kuomba msamaha. Chagua jibu sahihi kutokana na maelezo haya:
A. Leona alimwandikia Toni barua ya kuomba msamaha.
B. Leona aliandikiwa na Toni barua ya kuomba msamaha.
C. Leona alimwandikisha Toni barua ya kuomba msamaha.
D. Leona na Toni waliandikiana barua ya kuomba msamaha.

42. Usemi halisi wa sentensi, **Tiriki alitangaza kuwa vijana wangefaidika na miradi ya kujiendeleza mwaka huo,** ni
A. "Vijana watafaidika na miradi ya kujiendeleza mwaka huu," Tiriki alitangaza.
B. "Vijana wangefaidika na miradi ya kujiendeleza mwaka huo." Tiriki alitangaza.
C. "Vijana watafaidika na miradi ya kujiendeleza mwaka huo." Tiriki alitangaza.
D. "Vijana wangefaidika na miradi ya kujiendeleza mwaka huu," Tiriki alitangaza.

43. Chagua sentensi iliyo katika hali ya udogo.
A. Bwawa la mto huo linawafaa wakaaji wa kijiji hicho.
B. Kibwawa cha kijito hicho kinawafaa wakaaji wa kijiji chao.
C. Kibwawa cha mto huo kinawafaa wakaaji wa mji huo.
D. Bwawa la kijito hicho linawafaa wakaaji wa mji wao.

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

15273823

# BLANK PAGE

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com